

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA KUMI NA NANE**

**04 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 04 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **226. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Chikola na Makanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

##### **227. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya Geterer na Masieda.

##### **228. MHESHIMIWA DKT. PAULINA DANIEL NAHATO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Mabweni kwenye Shule za Wasichana wanaosoma Masomo ya Sayansi.

**229. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Km 10 kwa kiwango cha Iami Mjini Tunduma.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**230. MHESHIMIWA JANETH MAURICE  
MASSABURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja kupeleka Maofisa Usalama barabarani Falme za Kiarabu na Vietnam ili kujifunza jinsi ya kudhibiti ajali.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**231. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI  
(MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Jeshi la Uhifadhi litapata Kamishna Jenerali na kuleta muunganiko katika divisheni ya NCAA, TANAPA, TAWA na TFS.

## **WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

### **232. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Kituo cha Posta kilichopo Kengeja kitafanyiwa ukarabati na kutumika.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **233. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Kilombero baada ya Wananchi kutenga eneo la hekari 30.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **234. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (CHAANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia TBA kuwajengea nyumba Watumishi wa Serikali ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
04 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**